Australian Early Development Census
An Australian Government Initiative

NSW GOVERNMENT

**Australian Early Development Census (AEDC)**
**Frequently asked questions for families**

# Sensa ya Maendeleo ya Mapema ya Australia

## Maswali yanayoulizwa mara kwa mara kwa familia

### Sensa ya Maendeleo ya Mapema ya Australia (Australian Early Development Census (AEDC)) ni nini?

AEDC ni kipimo cha msingi wa idadi ya watu ya jinsi watoto nchini Australia wamekua wakati wanapoanza shule. Walimu wanakamilisha kifaa cha utafiti, toleo la Australia la Kifaa cha Maendeleo ya Mapema (Instrument) kwa kila mtoto katika darasa lao. Instrument inapima maeneo muhimu matano ya ukauaji wa utoto wa mapema:

- afya ya mwili na ustawi
- uhamiri wa kijamii
- ukomavu wa kihisia,
- ujuzi wa lugha na utambuzi (shuleni)
- ustadi wa mawasiliano na maarifa ya jumla.

Maeneo haya yanahusishwa karibu na vitabiri vya matokeo ya afya, elimu na kijamii ya watu wazima.

Serikali ya Australia imeidhinisha AEDC kama kipimo cha kitaifa ya ukuaji wa utoto wa mapema nchini Australia.

### Nani anawajibika kwa AEDC?

Serikali ya Australia na serikali za jimbo na wilaya zinafanya kazi kwa ushirikiano na mashirika mbalimbali kutoa AEDC. Kituo cha Utafiti wa Kijamii (Social Research Centre) huko Melbourne hukusanya na kusimamia data/takwimu za AEDC.

### Kwa nini data za AEDC zinakusanywa?

Thamani ya AEDC ni kuwa inatoa habari kwa shule, jamii na serikali. Habari hii inasaidia kutambua huduma, rasilimali na msaada kwa watoto na familia ili kusaidia kuunda siku zijazo na ustawi wa watoto nchini Australia.

AEDC pia inaweza kutumiwa kufuatilia mabadiliko katika ukuaji wa watoto katika jamii kwa muda ili kuelewa jinsi hali za mitaa zinapoweza kubadilishwa ili kuboresha nafasi za maisha ya watoto.

### Jinsi gani data za AEDC zinakusanywa?

Walimu wanakamilisha toleo la Australia la Kifaa cha Maendeleo ya Mapema (Instrument) (sawa na dodoso) kwa watoto katika mwaka wao wa kwanza wa shule ya wakati wote kwa kutumia mfumo salama wa kuingia. Instrument inakamilishwa kutegemea maarifa na uchunguzi wa mwalimu wa watoto katika darasa lake. Watoto hawahitaji kuwepo wakati walimu wanapokamilisha Instrument. Shule zinatolewa na fedha kwa muda wa misaada ya walimu – inachukua walimu takriban dakika 20 kwa mwanafunzi ili kukamilisha kila Instrument.

Inashauriwa wakati wa kukamilisha Instrument kwa mtoto wa Asili au wa Visiwa vya Torres Strait, mwalimu anapata ushauri wa Mshauri wa Utamaduni wa Watu wa Asili na wa Visiwa vya Torres Strait, inapowezekana. Washauri wa Utamaduni wa Watu wa Asili na wa Visiwa vya wanaleta maarifa ya kipekee ya kitamaduni na wamewekwa vizuri kuwasaidia walimu kukamilisha Instrument kwa sababu ya ufahamu wa kibinafsi wa njia za kujifunza na kutenda za watoto wa Asili au wa Visiwa vya Torres Strait.

### Je! Mwalimu wa mtoto wangu anapaswa kukamilishwa AEDC kwa mtoto wangu?

AEDC ni sensa muhimu, inayokamilishwa kitaifa ya ukuaji wa utoto wa mapema. Katika 2018, habari ilikusanywa kuhusu karibu watoto 309,000 katika mwaka wao wa kwanza wa shuleni. Inapokamilishwa, AEDC inatoa habari kwa jamii, wazazi, shule na serikali ili kugawia huduma, rasilimali na msaada ambao watoto wanahitaji kwa ufanisi zaidi.

Matokeo ya AEDC yanaunda muundo na matumizi ya mipango na sera za utotoni mapema kwa lengo la kuhakikisha watoto wanapewa mazingira salama, ya kujifunzia yenye kulea wanapoweza kukua na kustawi. Tunajua kuwekeza katika rasilimali kusaidia watoto katika miaka yao ya mapema kunaleta faida ya muda mrefu kwao na kwa jamii mzima. AEDC ni ya hiari, sio mtihani na mtoto wako hahitaji kuwepo. Mwalimu anakamilisha Instrument kulingana na uchunguzi wao na matokeo yanawekwa pamoja kama kundi ili faragha ya watoto, walimu na shule inadumishwa. Mtoto wako hatatambuliwa kwa binafsi katika data au ripoti.

Kabla ya kila ukusanyajii wa data wa AEDC unapoanza wazazi/walezi hupewa barua kuwafahamisha kama shule ya mtoto wao itashiriki au la. Wazazi/walezi wanaweza kuarifu shule wasipotaka mwalimu kukamilisha AEDC kwa ajili ya mtoto wao.

## Je! Naweza kupata matokeo ya mtoto wako kuondolewa kutoka hifadhidata ya ukusanyaji?

Ndio. Ni wazi kwako kuondoa idhini kwa ushiriki wa mtoto wako katika AEDC wakati wowote. Ikiwa unaondoa idhini yako, habari ya mtoto wako zitaondolewa kutoka hifadhidata ya ukusanyaji. Unaweza kufanya hivi kwa kuwasiliana na shule ya mtoto wako. Hata hivyo ikiwa unaondoa idhini yako baada ya data zimesharipotiwa, habari za mtoto wako haziwezi kuondolewa.

## Je! Habari za mtoto wangu zinahifadhi kwa usalama?

Ndio. Idara ya Elimu, Ustadi na Ajira (Department of Education, Skills and Employment (DESE)) ni msimamizi wa data ya AEDC na inatekeleza mbinu za ukusanyaji wa data, teknolojia za uhifadhi na utoaji wa taarifa ambazo zinahakikisha uaminifu na salama za data za AEDC. Kanuni za usalama (itifaki) zilizokubaliwa kati na DESE pamoja na watoaji wote wa huduma wenye mkataba zinahitaji ulinzi kudhidi upatikanaji isiyoidhinishwa na uharibifu kwa ajali na mabadilisho ya data za AEDC.

## Naweza kuwasiliana na nani ikiwa nina maswali zaidi juu ya faragha ya Habari za mtoto wangu au ningetaka kutoa lalamiko?

Maswali na malalamiko yote kuhusu faragha ya habari za AEDC yaelekezwa kwa DESE kwa maandishi kwa aedc@education.gov.au Pia kuna habari mbalimbali kwenye mpango wa AEDC unaopatikana kutoka tovuti ya AEDC www.aedc.gov.au

Tovuti ya DESE inajumuisha habari ifuatayo:

- Sera ya faragha ya DESE
- habari juu ya jinsi DESE inavyotii na Kanuni ya Faragha ya Australian (Australian Privacy Principles (APP))
- jinsi malalamiko ya ukiukaji uliotuhumiwa wa faragha yanaweza kutekelezwa
- maelezo ya jinsi DESE inavyoshughulikia na malalamiko.

## Je! Mtoto anapaswa kuwepo wakati mwalimu anapokamilisha toleo la Australia la Instrument?

Hapana. Walimu wanakamilisha toleo la Australia la Instrument kwa kutumia mfumo salama wa ukusanyaji wa data. Maswali yanajibiwa kulingana na maarifa ya mwalimu na uchunguzi wa watoto katika darasa lake. Sio mtihani na watoto hawahitaji kuwepo wakati walimu wanapokamilisha maswali yale.

## Je! Ripoti ya mwalimu ina uaminifu jinsi gani?

Ripoti ya mwalimu ni ya kuaminika sana. Utaalamu wa weledi ya walimu na ufahamu wa watoto wanaofundisha unamaanisha wapo wazuri kuchunguza ukuaji wa watoto.

Uchunguzi nchini Canada umehakikisha kuaminika kwa kuripoti ya mwalimu kwa kutumia walimu tofauti kuripoti kuhusu watoto hao hao.

Walimu wanapewa mwongozo wa kina na wanafanya mafunzo ya saa moja kuwasaidia kutumia Instrument hiyo kwa sahihi.

Walimu ni wataalumu wa ustadi mwingi wenye maarifa ya ukuaji wa utoto wa mapema. Hii inafanya wawe katika nafasi nzuri ya kuchunguza ukuaji wa watoto.

## Je! Wazazi/walezi watapata matokeo ya binafsi kwa mtoto wao?

AEDC sio kama Mpango wa Tathmini wa Kitaifa wa Kusoma na Kuhesabu (NAPLAN) ambapo taarifa za binafsi zinatolewa kwa wazazi/walezi. Kwa AEDC data za mtoto wako zitawekwa na data kutoka watoto wanaoishi katika jamii sawa. Matokeo ya AEDC kwa watoto wa binafsi hayaripotwi na AEDC haitumiwi kama kifaa cha kubainisha mtu binafsi. Hii inamaanisha kuwa ripoti ya mtoto wa binafsi haijatolewa.

Kwa habari zaidi kuhusu kupatikana habari ya mtoto wako tafadhali angalia tovuti ifuatayo Department of Education, Skills and Employment's Guide to Accessing and Correcting Your Personal Information.

## Je, AEDC amefanywa hapo awali?

Kati ya 2004 na 2008 AEDC ilijaribiwa katika jamii 60 kote Australia. Hii ilijumuishwa watoto 56,752, walimu 2,157 kutoka shule 1,012 (yote ya serikali na isiyo serikali) kutoka kila jimbo na wilaya (isipokuwa eneo la Northern Territory).

Katika 2009, AEDC (iliyojulikana zamani kama Kielezo cha Maendeleo ya Mapema ya Australia (Australian Early Development Index (AEDI))) kiliendeshwa kitaifa kwa mara ya kwanza, kikitoa picha ya matokeo ya ukuaji wa utotoni mapema ya watoto nchini Australia.

AEDC imeendeshwa kwa kitaifa kila miaka mitatu tangu ile (2012, 2015, 2018). Zaidi ya asilimia 95 ya shule zenye watoto wanaostahiki wameshiriki katika kila ukusanyaji.

## Kwa nini tutumie kipimo cha idadi ya watu?

Kipimo cha idadi ya watu kinazingatia idadi ya watu au vikundi. AEDC inachunguza ukuaji wa utoto wa mapema kote jamii mzima. Kuhamisha mwelekeo wa juhudi kutoka kwa mtoto binafsi kwa watoto wote katika jamii kunaleta tofauti kubwa kwa watoto wengi zaidi.

Data za AEDC zinaweza kutumiwa na jamii, shule, watengenezaji wa sera, walimu wa utoto wa mapema na huduma za kiafya, halmashauri za mitaa na serikali kushirikiana na rasilimali nyingine (kama takwimu ya jimbo na kitaifa) ili kupanga na kutathmini juhudi kusaidia ukuaji bora wa utotoni mapema.

## Je, Ni faida gani za AEDC?

Utafiti unaonyesha kuwa mapito na mahusiano ambayo watoto wachanga na watoto wanayo mnamo miaka yao ya mapema yanathiri sana maendeleo yao ya baadaye. Kutoa aina nzuri ya huduma, rasilimali na msaada mnamo miaka ya mapema huleta faida ya maisha mzima kwa watoto na jamii.

Walimu katika Australia waliripoti kwamba kushiriki katika AEDC kuliongeza ufahamu wao wa mahitaji ya watoto wa binafsi na darasa kwa ujumla. Pia waliripoti pia kwamba kukamilisha AEDC ilisaidia kupanga kwao kusaidia mabadiliko ya watoto kwenda shuleni na mipango ya darasa.

Fedha zinazoendelea za AEDC zinahakikisha serikali na jamii ziendelee kuwa na maelezo zinayohitaji ilikufanya utofauti katika maisha ya watoto wadogo na familia zao. Ushirikiano ambao umeshakua tayari kote huduma za elimu, afya na za jamii unaweza kuendelea kukua na kujenga juu kazi ambazo zimeshaanzisha.

Matokeo kutoka makusanyanyo ya data yaliopita yametumiwa kusaidia watoto wadogo na familia zao kwa njia anuwai:

- jamii zimeanzisha viwanja vipya vya kuchezea na huduma za uzazi
- shule zikiona kuboreshwa kwa ufaulu wa wanafunzi kupitia programu mpya za kusoma na kuandika
- serikali kutumia data kama ushahidi wa kuunda sera bora kwa watoto.

Kwa mifano ya jinsi gani matokeo ya AEDC yametumiwa na shule na jamii, tafadhali angalia kwa hadithi kweli za shule (school stories) na hadithi kweli za jamii (community stories) kwenye tovuti za AEDC.